***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...***

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika hafla hii ya utoaji wa **Tuzo ya Mwajiri Bora wa Mwaka 2022.** Napenda pia kuwashukuru kwa dhati wenyeji wetu, Chama cha Waajiri Tanzania, kwa kuona umuhimu wa kumualika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mgeni Rasmi kwenye sherehe hii. Hata hivyo, kutokana na majukumu mengi ya kitaifa aliyonayo, imempendeza Mheshimiwa Rais kunituma nimwakilishe.

Mheshimiwa Rais, ameniagiza niwaambie kwamba anatambua kazi nzuri ya Waajiri nchini na anathamini mchango wenu katika kutoa ajira kwa Watanzania. Aidha, Mheshimiwa Rais anawahimiza kuendelea kushirikiana na serikali katika kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi na pia kulipa kodi stahiki kwa maendeleo ya nchi yetu.

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***
Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza kwa dhati waandaji wa tuzo hizi muhimu. Nafahamu kwamba kwa miaka miwili mfululizo (2020 na 2021) hamkuweza kutoa Tuzo hizi za Mwajiri Bora wa Mwaka kutokana na Janga la UVIKO -19 lakini mwaka huu mmeweza kufanikisha utoaji wa Tuzo hizi. **Hongereni sana!** Aidha, niwapongeze pia kwa kushirikiana na Serikali kipindi chote cha janga la UVIKO-19 na pia kwa kutoa miongozo mbalimbali ya kuwasaidia Waajiri kuvuka salama bila kuvunja Sheria za nchi na kuhakikisha ustawi wa wafanyakazi, huku mkipunguza athari za janga hilo.

Nimefurahi kusikia kwamba mlitumia kipindi hicho cha miaka miwili kufanya marejeo ya uboreshaji wa mchakato wa utoaji wa Tuzo hizi katika vipengele mbalimbali ikiwemo: **Namna ambavyo makampuni yanakabiliana na Majanga yanayotokea katika Maeneo ya Kazi mfano Janga la UVIKO 19; Mabadiliko ya Tabianchi; Usawa wa Kijinsia na Usawa katika Maeneo ya kazi; na kipengele cha Kufuata Miongozo na matakwa ya Kisheria**. Kwa hakika vipengele hivi ni muhimu sana na vinaendana na vigezo vya kimataifa na wakati tuliopo hivi sasa. Kwa Uzoefu tuliopata kipindi cha UVIKO-19, ni dhahiri Waajiri hamna budi kujipanga na kuweka mikakati madhubuti ya kukabiliana na majanga mbalimbali yanapotokea bila kuathiri uzalishaji na huduma zinazotolewa. Aidha, mnao wajibu wa kuhamasisha

uwepo wa rasilimali watu inayozingatia usawa wa kijinsia na kuwajengea uwezo wanawake katika masuala ya uongozi. Jambo hili ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii na Taifa letu kwa ujumla kwani tunaamini mazingira yenye usawa ni motisha kubwa kwa wafanyakazi. Kadhalika, mmefanya vyema kuwa na kipengele kinachohusiana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa sababu ninaamini kitasaidia kwa kiasi kikubwa kuhamasisha makampuni na taasisi mbalimbali kubuni mikakati na mbinu endelevu za kuhifadhi na kutunza mazingira yetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadae.

***Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***
Natambua juhudi mbalimbali za ATE katika kuhakikisha kuwa Waajiri na waajiriwa kila mmoja kwa nafasi yake anatimiza wajibu wake mahali pa kazi. Mmekuwa mkitoa mafunzo kuhusu sheria za kazi na usimamizi wa Rasilimali Watu ambapo naamini mafunzo yamesaidia kupunguza migogoro mahali pa kazi na hivyo kujenga mazingira tulivu ya kufanya kazi. Aidha, natambua juhudi zenu katika kutoa mafunzo mahususi na kuhakikisha kunakuwa na nguvukazi yenye ujuzi na tija kubwa. Hivyo, kupitia hafla hii, napenda kutoa rai kwa waajiri kuwawezesha wafanyakazi kuhudhuria mafunzo mbalimbali yanayotolewa na ATE ambayo yatawawezesha kupata uelewa zaidi, kukidhi vigezo katika mazingira ya biashara, kufanya kazi kwa ufanisi na hatimae kuongeza uzalishaji. Vilevile**,** napenda kuwasihi Waajiri kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza ujuzi hususan kwa vijana wetu. Natoa rai kwenu kuendelea kutoa nafasi kwa wahitimu kujifunza kwa vitendo kupitia mafunzo tarajali (*Internship*) na Uanagenzi *(Apprenticeship).* Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali kwa upande wake, itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi kutoka ndani na nje ya nchi kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu.

Nawapongeza pia ATE kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha Masuala ya Afya na Usalama mahala pa kazi. Nimeelezwa kuwa mmefanya Bonanza la waajiri kwa mara ya kwanza lenye kaulimbiu isemayo "**Wafanyakazi Wenye Afya ni Mtaji"** kwa lengo la kuhamasisha na kuelimisha umuhimu wa afya na usalama mahala pa kazi. Sisi sote tunafahamu kuwa, ili Taifa liweze kuwa na uchumi imara, ni lazima kuwa na nguvukazi yenye afya njema na kwamba michezo ni njia moja wapo inayoweza kutumika kuhakikisha tunafanikisha lengo hilo. Hapa nchini, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya inaonekana kuwa wafanyakazi, hususan wa maofisini, tuko kwenye hatari kubwa ya kupata magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari na shinikizo la damu; ambayo kwa kiasi kikubwa husababishwa na kutofanya mazoezi mara kwa mara. Hivyo, hatuna budi kusisitiza wafanyakazi kufanya mazoezi mara kwa mara katika Taasisi

zetu. Kwa muktadha huu, nawapongeza sana kwa kufanya Bonanza hiyo na yafaa mwendeleze utaratibu huu wa kutumia michezo kujenga afya za waajiri pamoja na waajiriwa ili kwa pamoja walete tija katika uzalishaji. Aidha, kupitia jukwaa hili napenda pia kuhamasisha mashirika na taasisi mbalimbali kujiunga na Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi Nchini (SHIMMUTA) ili kwa pamoja tuwe na utaratibu mzuri utakaotuwezesha kufanya mazoezi, kuleta umoja na ushirikiano kati yetu.

**Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**
Napenda kutumia nafasi hii kuwaasa waajiri na waajiriwa kote nchini kuzingatia yafuatayo:

**Jambo la Kwanza**; kutoa haki na stahili za wafanyakazi wenu kwa mujibu wa mikataba yao ya kazi. Ofisi yangu imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi mbalimbali walioachishwa kazi, kuchelewa au kudhulumiwa haki zao bila kufuata sheria. Tukumbuke kuwa, haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa. Hivyo, tunapoadhimisha sherehe hizi za mwajiri bora, nawakumbusha waajiri wote kutenda haki kwa kuzingatia sheria zetu za kazi.

**Jambo la Pili**, Nawataka waajiri kuzingatia sheria zilizopo kuhusu ajira kwa wageni. Ninafahamu kuwa baadhi ya waajiri wamekuwa wakiajiri wageni hata katika nafasi zisizo za kitaalam au ambazo utalaam wake unaweza kupatikana hapa nchini. Nataka Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na timu yako muwe mnafuatilia taarifa hizo na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi. Kwa kazi zinazohitaji wataalam kutoka nje (*expatriates*), nawasisitiza waajiri kutekeleza mpango wa kuandaa wataalam wazawa watakaochukua nafasi hizo baada ya mikataba ya wataalam hao kuisha muda wake kama sheria inavyoelekeza. Wizara endeleeni kusimamia suala hilo.

**Jambo la Tatu**, ninawahimiza waajiri muendelee kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na tija yao katika uzalishaji. Kama nilivyoeleza, Serikali imeondoa baadhi ya tozo zilizokuwepo ili kuboresha mazingira ya uzalishaji na kuongeza tija. Kwa ajili hiyo, waajiri angalieni pia namna mtakavyoweza kuboresha maslahi ya wafanyakazi wenu. Nawasihi sana kuangalia njia mbalimbali za kuwawezesha waajiriwa kujikimu na kukabiliana na hali halisi ya uchumi ikiwa ni pamoja na kutoa posho, tuzo na motisha mbalimbali ili kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi bora katika taasisi zenu, kuwapandisha vyeo na kuwapatia stahili zinazoendana na nafasi zao.

**Jambo la Nne**, ni kuhusu mikataba. Ninawakumbusha waajiri wote kuzingatia sheria na kutoa mikataba ya kazi kwa kazi zinazostahili mikataba badala ya kuwafanyisha watu kazi kama vibarua kwa kazi ambazo wangeweza

kupata mikataba ya kazi. Aidha kwenye hili pia, naiagiza Wizara ya Kazi kutoa elimu kwa waajiriwa kujua haki zao na pia kuhakiki aina ya mikataba inayotolewa ili ikidhi vigezo vyote muhimu ikiwa ni pamoja na kuainisha wajibu na haki za mwajiri/mwajiriwa kwenye masuala ya afya, likizo, ulemavu, mafao, migogoro n.k

**Jambo la Tano**, napenda nisisitize suala la kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuhakikisha wanapewa vitendea kazi vinavyohitajika ili kuweza kufanya kazi vizuri na kwa usalama. Aidha, Waajiri wote hawana budi kuwa na mipango mahususi kwa kila kada kila mwaka ambayo itawezesha waajiriwa kujinoa kitaaluma ili waweze kufanya kazi kwa ubora na ufanisi unaotegemewa na waajiri. Vilevile, ni muhimu kuhakikisha wafanyakazi wanapata vitendea kazi stahiki kulingana na mazingira ya kazi kama vile kompyuta na vifaa kinga (*protective gears*).

**Jambo la Sita,** napenda kuwakumbusha waajiriwa kuwa, Serikali inategemea kuona nguvukazi yenye uzalendo, utendaji bora, uadilifu na ufanisi katika fani mbalimbali. Nawakumbusha kwa msisitizo mjiepushe kabisa na vitendo vya rushwa, ufisadi, na kuhujumu uchumi wa nchi yetu. Ni lazima sisi sote tufuate sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika utendaji wetu.

**Jambo la Saba na la mwisho**, ni kuhusu vitendo vya uonevu, unyanyasaji na ukatili kazini. Kumekuwa na tabia ya uonevu au dhuluma kwa wafanyakazi na matumizi mabaya ya madaraka ambayo husababisha wafanyakazi kudhalilishwa na kuwa wanyonge mahali pa kazi. Halikadhalika, tumeshuhudia pia waajiriwa kunyanyaswa kwa ajili ya umri, jinsia, rangi, kabila, ulemavu au dini zao. Vitendo hivyo ni ukiukwaji wa haki za binadamu na vinaathiri utendaji wa kazi sio tu kwa waathirika, bali kwa viongozi na Taasisi au Mashirika wanayofanyia kazi. Ni lazima tuhakikishe vitendo hivi vinakomeshwa katika taasisi zetu. Kila mfanyakazi ana haki ya kutendewa utu, kuthaminiwa na kuheshimika kazini. Lazima tuweke mifumo itakayowezesha wafanyakazi kutoa taarifa za kunyanyaswa au kuonewa bila kuhofia madhara yoyote yanayoweza kujitokeza ikiwemo kupoteza ajira zao.

**Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**

Nafahamu hapa wapo wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Umma na Makampuni Binafsi. Ni vema pia nitumie fursa hii kuwakumbusha wajibu wenu wa kuchangia shughuli za maendeleo kwa jamii inayowazunguuka; na kutoa gawio kwa wanahisa wenu ikiwa ni pamoja na Serikali. Yapo Makampuni na Mashirika ya Umma ambayo kwa kweli yanajitahidi sana kutoa mchango wao kwa jamii inayowazunguka na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Sitayataja hapa lakini tunayafahamu na sisi Serikali

tunawashukuru sana. Natoa rai kwa wale ambao hawajaanza kutoa michango yao kwa jamii inayowazunguka au kuchangia jitihada za Serikali katika maendeleo waanze kufanya hivyo mara moja.

**Ndugu Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**
Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwapongeza sana ATE kwa kuhakikisha mchakato wa kutafuta washindi unakuwa wa wazi na hivyo kuzipa tuzo hizi heshima ya hali ya juu. Vilevile, nawapongeza waajiri wote walioshiriki katika kuwania tuzo hizi, hususan Mwajiri atakayeshinda Tuzo ya Mwajiri Bora wa Mwaka 2022. Niwasihi sana kuzifanya tuzo hizi kuwa chachu ya kuboresha mazingira ya mahali pa kazi na kuhamasisha utendaji wenye tija kwa manufaa ya taasisi zenu na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Aidha, ninawahakikishia kuwa kupitia utatu wetu kwa maana ya Serikali, Vyama vya Waajiri na Vyama vya wafanyakazi, tuko tayari kuendelea kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu Ajira na Kazi nchini ili kuboresha na kutatua changamoto zilizopo kwa pamoja. Kwa upande wa Serikali chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumejipanga kuhakikisha sheria na sera za nchi zinakidhi mahitaji ya waajiri na waajiriwa. Vilevile, Serikali inaendelea kuwajengea uwezo watumishi na pia kuboresha mazingira na mitaala ya Vyuo vyetu ili iendane na maendeleo ya sanyansi na teknolojia na pia tunaongeza idadi ya shule na vyuo katika mikoa yetu yote ili wananchi zaidi wapate fursa ya kujiendeleza kimasomo na kupata elimu ambayo itawawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**Ndugu Washiriki;** napenda nimalizie kwa kusisitiza kuwa, pamoja na kutafuta mshindi wa tuzo ya leo, tutumie fursa hii kufahamiana na kujenga mtandao wa kibiashara; maana hapa pia ni sehemu sahihi ya kubadilishana uzoefu kuhusu namna nzuri ya kuimarisha umoja wetu.

**Baada ya kusema hayo, ninawatakia utendaji uliotukuka mtakaporudi kwenye maeneo yenu ya kazi. Na sasa niko tayari kutoa TUZO YA MWAJIRI BORA WA MWAKA 2022!**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**